

Muhtasari wa Mwenendo wa Mvua kwa Siku 10 Zilizopita na Matarajio kwa siku 10 Zijazo

1.0 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 01-10 OKTOBA, 2026 NA MATARAJIO YA MVUA KWA TAREHE 11-20 OKTOBA, 2026

1.1 MUHTASARI WA MWENENDO WA VIASHIRIA NA MIFUMO YA MVUA TAREHE TAREHE 01-10 OKTOBA, 2026.

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) iliimarika kidogo, wakati ile iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) ilidhohofika kidogo. Hali hii ilisababisha sehemu ya ukandamvua kusogea kidogo kuelekea kusini hadi katika maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria, Magharibi mwa nchi na baadhi ya maeneo ya nyanda za juu kusini magharibi. Vilevile, joto la bahari katika eneo la magharibi mwa bahari ya Hindi (pwani ya Africa Mashariki) lilikuwa la juu ya wastani kuliko lile la eneo la mashariki mwa Bahari ya Hindi (pwani ya Indonesia). Hali hii iliimarisha kuvuma kwa upepo wenye unyevunyevu kutoka baharini kuelekea maeneo ya ukanda wa pwani ya nchi yetu na yale ya nyanda za juu kaskazini mashariki na hivyo kuimarisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo hayo.

1.2 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 01-10 OKTOBA, 2026

Viashiria vilivyotajwa hapo juu vilipelekea vipindi vya mvua zinazoambatana na ngurumo za radi katika maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria na Magharibi mwa nchi; na vipindi mvua viliripotiwa katika maeneo ya ukanda wa pwani, nyanda za juu kaskazini mashariki pamoja na nyanda za juu kusini magharibi.

2.0 MATARAJIO YA HALI YA HEWA KWA TAREHE 11-20 OKTOBA, 2026

2.1 VIASHIRIA NA MIFUMO YA MVUA KWA TAREHE 11-20 OKTOBA, 2026

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) inatarajiwa kuendelea kuimarika, wakati ile iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuendelea kudhohofika. Hali hii inatarajiwa kusababisha sehemu ya ukanda mvua (ITCZ) kusogea kidogo kuelekea kusini, na kuwepo katika maeneo ukanda wa Ziwa Victoria na magharibi mwa nchi. Vilevile, joto la bahari katika

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Kiwanja Na. 6, Kitalu "N", Mtaa wa Fahmida, Dodoma jiji,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe: met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

eneo la magharibi mwa bahari ya Hindi (pwani ya Africa Mashariki) linatarajiwa kuwa la juu ya wastani kuliko lile la eneo la mashariki mwa Bahari ya Hindi (pwani ya Indonezia). Hali hii inatarajiwa kuimarisha kuvuma kwa upepo wenye unyevunyevu kutoka baharini kuelekea maeneo ya ukanda wa pwani ya nchi yetu na yale yaliyoko nyanda za juu kaskazini mashariki na hivyo kuimarisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo hayo.

2.2 MWELEKEO WA HALI YA HEWA KWA TAREHE 11-20 OKTOBA, 2026

Kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara): Vipindi vya mvua zinazoambatana na ngururumo za radi vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo.

Nyanda za juu kaskazini-mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro): Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache.

Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba): Vipindi vya Mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo.

Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora): Vipindi vya mvua zinazoambatana na ngururumo za radi vinatarajiwa katika maeneo machache, hususan katika mkoa wa Kigoma.

Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida): Hali ya ukavu inatarajiwa.

Nyanda za juu Kusini-magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa): Hali ya ukavu kwa ujumla inatarajiwa.

Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi): Vipindi vya mvua nyepesi vinatarajiwa katika maeneo machache.

Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro): Hali ya ukavu inatarajiwa.

Imetolewa na:

MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Kiwanja Na. 6, Kitalu "N", Mtaa wa Fahmida, Dodoma jiji,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe: met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz